# Learning by Ear – Religious Dialogue: "A Bridge over Gori"

# Episode 05: "Mjadala Motomoto"

**Author: Romie Singh**

**Editors: Katrin Ogunsade, Naïma Guira**

**Proof reading: Natalie Glanville-Wallis**

**Expert on African religions: Jean-Félix Belinga Belinga**

**KISUAHELI ERIC PONDA**

**List of characters for episode 5:**

- Narrator /Philip, male (17)
- Harry, male (17)
- Mat, male (16)
- Layla, female (16)
- Roshi, female (16)
- School director, Mrs Milulu, female (48)
- Father Barnabus Dembele, Harry's uncle (49)
- Philip's father, Layton-Brown (50)
- Hassan, Layla's brother (12)
- + Students in the background

1. **SIG TUNE UP**

2. **INTRO:**

**Hujambo na karibu kwa sehemu ya tano kwenye mfululizo huu wa vipindi vya Noa Bonga Jenga maisha yako, tukiwa bado katika Makala ya"Daraja la Gori" . Hadithi ya kusisimua kuhusu jinsi Dini na Siasa zinavyoweza kuzua uhasama na migongano baina ya jamii mbili na kadhalika Familia Mbili Mjini Gori.Katika makala ya leo,siku iliyosubiriwa kwa hamu ya uzinduzi wa kundi la mjadala na mdahalo katika Chuo Cha Ubuntu imefika. Kila mmoja ameshikwa na msisimko shuleni humo. Lakini pia kuna habari za kushangaza zinazosababisha huzuni na kutoelewana hasa katika uhusiano mpya wa mapenzi kati ya mabingwa wetu wachanga Harry na Layla.Msimulizi wa kisa chote ni Philip ambaye ni mmoja wa marafiki wa dhati wa Harry.. Natumai utakuwa nasi hadi tamati ujue zaidi.**

**Scene 1. At Ubuntu College**

**Director Milulu, Philip narrator, students in the background**

3. **SFX: Morning Assembly. Students and teachers sing Ubuntu Anthem (ending)**

**4. DIRECTOR:** Habari za asubuhi nyote! . Ni wakati mwengine tena tumekusanyia hapa kwa mkutano wetu wa asubuhi.

**5. ALL:** Ndio Bi Milulu.

**6. DIRECTOR:** Kama mujuavyo Jina la shule yetu UBUNTU linaashiria wazo la mababu zetu wa Kiafrika. Ubuntu maana yake hasa ni, huruma, kumjali mwenzio na pia kusadiana kwa hali zote .Kuwakumbusha tu filosofia yetu ya kuvumiliana na kuheshimiana, sasa tuombe dua..! Sitawaeleza iwapo dua hiyo ina misingi ya Kitamaduni,Kikristo au Kiislamu. Ikiwa itaigusa nafsi yako basi hilo ndilo la msingi.

**7. STUDENTS+DIRECTOR (reading prayer):**

**Ewe Roho mtakatifu, unayetoa uhai kwa viumbe wote ulimwenguni, sikiza ombi langu. Nahitaji nguvu na busara yako.Naziomba nguvu ili nipambane na adui mkubwa zaidi- nafsi yangu wala sio kumdhalilisha mwenzangu.**

**Niwezeshe kuja kwako na mikono safi na bila woga ili mauti yakinijia nije kwako bila aibu.**

**8. <u>SFX: Murmur of students clearly moved</u>**

**9. DIRECTOR:** **Je dua hiyo imeigusa nafsi yako?**

**10. <u>SFX: All murmur in approval.</u>**

**11. DIRECTOR:** **Dua hiyo liliandikwa na Mmarekani asilia-Chifu Yellow Lark mwaka 1887.**

**12. <u>SFX: All murmur in approval</u>**

***13.*** **DIRECTOR:** **Sasa la msingi ni kusameheana.Lazima kwanza tuheshimiane na kuishi pamoja kwani tu Wanadamu kwanza kasha wawakilishi wa madhehebu fulani.. Kwa hivyo sheria ya kupiga marufuku mavazi au nembo zozote zinazoashiria dini fulani bado inadumishwa hapa shuleni .Hata hivyo Wanafunzi wa Kiislamu wameomba**

**waruhusiwe kuvaa mavazi ya mikono mirefu na suruale ndefu pamoja na hijabu wanaposhiriki michezoni nje ya shule yetu ambako kuna watu wengine wanaoitazama michezo.Wanafunzi hao wamesema kuwa wanataka kushiriki kwenye michezo hiyo kwahiyo lazima tulitafutie suala hilo suluhu.Nitaliwasilisha suala hilo la mavazi mbadala ya michezo katika mkutano wa ujao wa magavana wa shule.**

***SFX: Murmur of approval among students***

**14. DIRECTOR:** **Kadhalika kundi la mjadala na mdahalo linazinduliwa rasmi leo mwendo wa saa tisa alasiri. Ntawaomba muhudhurie ufunguzi huo ndipo muijue mada ya kwanza itakayojadiliwa! Sina mengi ila kuwatakia siku njema.**

**AMBIENCE FADE OUT**

**15. PHILIP/NARRATOR: Siku yangu ingekamilika au kuwa nzuri vipi?Nilihisi Layla kamwe hakuniona.Nilienda kwenye ukumbi wa mjadala ili tu niwe karibu naye. Lakini machoni mwake , mimi nilikuwa kama watu wengine katika mkusanyiko huo.**

**Scene 2. At the Debating Club**

**Harry, Layla, Mat, Philip, Roshi, groups of boys and girls**

**16. SFX: Students in classroom. Excited chatter (fade out)**

**17. HARRY: Habari za mchana nyote. Nafurahi kuona mumefika kwa wingi katika hafla hii ya uzinduzi wa kundi letu la Mjadala na Mdahalo.Mwenyekiti wetu ni Layla na tunampa fursa hii azungumze machache..**

**18. LAYLA: Ahsante Harry.. Mkurugenzi wa Chuo ameturuhusu tutumie ukumbi huu kwa muda wa dakika 45.Tunahitajika kuwa na muongozo kwahivyo nawaomba mutoe mapendekezo yenu kisha nitayanakili.**

**19. MAT:** **Kutochelewa!**

**20. PHILIP:** **Kuheshimu maoni ya wengine!**

**21. SFX: Cell phone rings**

**22. ROSHI:** **Simu zote zizimwe wakati wa mjadala *(laughter)***

**23. LAYLA:** **Sawa. Kila anayetaka kuzungumza anyoshe mkono:Tafadhali usimkate mwenzako kauli. Maada kuu iliyopewa uzito zaidi ni ile ya Ndoa ya Mitala, yaani kuoa wake wengi. Tukianza , labda niulize tunakifahamu kipi kuhusu ndoa hii ya mitala? Naam Roshi?**

**24. ROSHI:** **Ni tamaduni iliyotumika tangu enzi za mababu zetu na inawapa wanaume umuhimu zaidi-unaowawezesha kuoa zaidi ya Mke mmoja!ila mwanamke haruhusiwi kuolewa na zaidi ya mume mmoja.Kulingana na mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za binadamu, sote…wake kwa waume.. tuna haki sawa.**

**25. MAT:** **Haki za nini? Kuiga wanaume? Huo ni upuzi mtupu.**

**26. ROSHI:** **Ni kweli Mat! Sasa kwanini wanaume wanaruhusiwa kufanya hivyo?**

**27. MAT:** **Ni utamaduni, Roshi. Watu wamekuwa wakiufuata utamaduni huu tangu jadi,pengine kama njia moja ya kuhakikisha kuwa unapata watoto wengi.**

**28. LAYLA:** *(raising her voice)* **Tafadhali nyosha mkono wako kabla ya kuzungumza…Umm.. Philip….?**

**29. PHILIP:** **Ninavyofahamishwa ni kwamba, tabia ya wanaume kuoa wake wengi ni kama bima kwa wazazi ili watoto wanaowazaa waweze kuwatunza wakati wa uzeeni.**

**30. MAT:** **Ni kweli, na pia kwa jamii za wakulima, hii ni njia moja ya kuongeza nguvu zaidi shambani na hata kwenye ufugaji pia. Sidhani hilo lina mjadala.**

**31. ROSHI:** **Kwanini halina mjadala!.** ***(laughter)*** **Huu ni ukumbi wa majadiliano!**

**32. <u>SFX: General laughing and clapping specially from the girls</u>**

**33. GIRLS:** **Kweli Roshi**!

**34. LAYLA:** **Tafadhali …. ...shhh. Ningependa kuuliza: Usawa wa kijinsia una uhusiano gani na utamaduni wa kuoa wake wengi?.**

**35. ROSHI:** **Hakuna uhusiano wowote!**

**36. <u>SFX: Girls roar approval. Noisy exchanges</u>**

**37. LAYLA:** ***(shouting above the noise)*** **Sawa…. Sawa, tuelewane tafadhali… hilo mosi. Je kuna jengine?**

**38. MAT:** ***(still shouting)*** **Waislamu huoa wake wengi.**

**(In quick succession:)**

**39. LAYLA:** **Babangu hana wake wengi.**

40. **ROSHI:** **Hata babangu hana pia**.

41. **MAT:** **Sawa sawa, tuseme baadhi ya wanaume wa Kiislamu huoa wake wengi.**

42. **ROSHI:** **Hata wanaume Wakikristo pia. Hili linafanyika kila mahali. Liko Marekani, Ulaya, sio hapa Barani Afrika pekee.Kwa huko wanalipa jina tofauti…anasema ana mpenzi wa kando au uhusiano wa pembeni.**

43. **SFX: Noisy disagreement/agreement**

44. **HARRY:** **Nyamazeni!... tusikilizane tafadhali.**

45. **SFX: People say shhh**

46. **HARRY:** **Kama mmoja ya wasimamizi wa mjadala huu, ningependa kuieleza tofauti baina ya ndoa za wake wengi na kuwa na uhusiano nje ya ndoa.Haya ni mambo mawili tofauti**.

47. **Room goes quiet.**

**48. HARRY:** **Mwanamume anayetaka kuoa mke wa pili au zaidi sharti apate ridhaa ya mke wake wa kwanza, ukizifuata tamaduni za Kiafrika. Ni wajibu wake kumtimizia mahitaji yake, amjengee nyumba.Ni tofauti kabisa na uhusiano wa mapenzi wa kando.Mwanamke au mwanamume anakuwa na uhusiano wa pembeni wa siri mbali ya ule wa ndoa rasmi. Ndoa ya Mitala ni tofauti!.japo ina kanuni zake.**

**49. ROSHI:** **Ndio udhibiti wa mwanamume!**

**50.** SFX: UPROAR AGAIN. FADE on voices/ clapping and disagreement from the students

**51. LAYLA:** **Shh – Nyamazeni… Kama kundi la mjadala tunahitaji kuwa na kauli ya pamoja inayowakilisha misimamo yote.Ndio maana nauliza:.. Je mnakubaliana na utamaduni huu wa Kiafrika wa kuoa wake wengi kama moja ya tamaduni za kiafrika za kisasa?**

**52. ROSHI:** **Hapana. Kamwe haukubaliki. Ukweli ni kwamba mwanamume hataki kukubali kuwa anapooa mke mwengine hilo linamuumiza mke wake…amini usiamini hilo humuumiza moyo Mwanamke kwa kweli.**

**53. <u>SFX: More noise and disagreement</u>**

**<u>AMBIENCE FADE UNDER</u>**

**54. PHILIP/NARRATOR:** **Mambo aliyoyasema Roshi kwa kweli yalinigusa.Baada ya mjadala nilisubiri nje ya ukumbi wa mjadala angalu niweze kuzungumza na Layla.Kwa bahati mbaya alikuwa na mazungumzo marefu na Harry na nikaamua kwenda kumsubiri nyumbani kwao.Nilitumai kwamba angefika baada ya muda mfupi ,lakini wapi. Mtu niliyemuona ni mdogo wake Hassan aliyetoka nje akiwa na chupa mkononi.Nilikata tamaa na nikaamua kwenda nyumbani baada ya kukutana na rafiki zangu katika mkahawa wa Reunion. Nilipofungua mlango Mtu wa kwanza niliye muona ni Babangu aliyechangamka kupita kiasi.**

**<u>Scene 3. At the Layton-Browne's</u>**

**Layton-Browne, Philip**

**<u>FADE IN P's FATHER: Talking fast on the telephone</u>**

**55. P'FATHER:** **Badilisha kichwa cha habari hizi. Badilisha. Weka."Kanisa jengine lateketezwa moto". Tumia kichwa hicho.**

**56. <u>SFX: banging telephone receiver</u>**

**57. P's FATHER:** **Habari..Philip.. Mambo siku hizi yanafurahisha**!

**58. PHILIP:** **Kwanini ?Kumetokea kipi Baba?**

**59. P'S FATHER:** **Hah! Unazungumza na mimi! Babako Layton Browne! Ni habari motomoto na gazeti la Gori ndilo litakalokuwa la kwanza kuzichapisha habari hizi pamoja na majina ya wahalifu.**

**60. PHILIP:** **Moto??Umetokea wapi?**

61. **P's FATHER:** Kwenye **kanisa la Mtakatifu Thomas. Hebu tazama mwandishi wetu wa habari wameipiga picha hii ya mvulana huyu kabla ya kubebwa na gari la Wagonjwa.**

62. **PHILIP:** **Picha?, hebu nione!**

63. **<u>SFX: Mouse click(showing photo on laptop)</u>**

64. **P's FATHER:** **Umemtambua, sivyo? Hata mimi namjua! Lazima nimfahamishe Kasisi Barnabus,aliyehusika na kitendo hiki cha kuliteketeza kanisa lake**!

65. **<u>SFX: Phone dialling and ringing then fade out</u>**

66. **PHILIP/NARRATOR: Baba aliichukua simu na kumpigia Babake Mdogo Harry, Kasisi Barnabus. Mimi nilisimama wima nimeduwaa. Picha hiyo ilimuonyesha bayana mhusika wa kitendo hicho, Nywele na Fulana aliyokuwa amevaa..**

**<u>Scene 4. At Harry's home</u>**

**Father Barnabus, Harry**

**<u>FADE IN CONVERSATION</u>**

**67. FATHER B:** ***(agitated. On the phone)*** **Aka!.....? Kumbe…... Ahsante sana kwa kunifahamisha.**

**68. <u>SFX: Hanging up telephone</u>**

**69. HARRY:** ***(nervous)*** **Ni nini Baba Mdogo?**

**70. FATHER B:** ***(furious)*** **Aha- Harry! Sasa nimekupiga marufuku kuonana na Layla Omer baada ya Shule.Unataka kujua ni kwanini? Ungetaka kujua? Kuna Mtu aliyejaribu kuliteketeza kanisa letu lililoko barabara kuu. Na unataka kumjua mhusika? Ni Hassan Omer mdogo wake Layla !Wakati huo ulikuwa unajishughulisha na Dadake.**

**71. HARRY:** **Jamani! Eti Hassan?**

**72. FATHER B:** **Layton-Browne *(mocking)* - Layton na herufu 'a', Browne na herufu 'e' –kutoka Gori ameipata picha ya mvulana huyo Hassan.Ohh! hii familia ya Omer!Kamwe hatuwezi kukubali iendelee kufanya vituko hivi.Na kuanzia leo, wewe…!... wewe, lazima utii amri yangu! Hakuna tena kutangamana na yule msichana wa Kiislamu ukitoka shule, umesikia Harry? Sitaki kukuona tena!**

**73. <u>SIG TUNE UP</u>**

**74. OUTRO:**

**Hadi hapo tunafika mwisho wa kipindi cha Noa Bongo-Jenga Maisha Yako kwa leo. Uhasama baina ya Wakristo na Waislamu unazidi kuongezeka katika mji huo wa Gori, baada ya kanisa la kasisi Barnabus kutiwa moto. Ungana nasi tena kwa makala nyengine ya Noa Bongo-Jenga Maisha Yako wakati tutakapoendelea na hadithi hii ya Daraja la Gori. Katika makala hiyo tutasikia jinsi Harry anavyojaribu kuyatuliza mambo. Ukiwa na maoni au ukipenda kusikiliza tena makala hii na vipindi vyengine vya Noa Bongo-Jenga Maisha yako, tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine Kwaheri kwa sasa!**

**END OF EPISODE 5**